East African Scholars Journal of Education, Humanities and Literature
OPEN ACCESS
*Abbreviated Key Title: East African Scholars J Edu Humanit Lit*
ISSN: 2617-443X (Print) & ISSN: 2617-7250 (Online)
Published By East African Scholars Publisher, Kenya
Volume-5 | Issue-4 | Apr- 2022 | DOI: 10.36349/easjehl.2022.v05i04.003

Review Article

# Ushairi WA Kiganda Unavyoweza Kuchangia Na Kuendeleza Ushairi WA Kiswahili Kimtindo Na Kimaudhui: Mfano WA Ufundishaji Nchini Uganda

Atukunda Edwine[1*], Dkt. Deborah Amukowa[2], Dkt. Owen McOnyango[2]

[1]Postgraduate Student, Maseno University, Kondele Kisumu-Busia Rd Maseno, Kisumu, Kenya
[2]Department of Kiswahili and Other African Languages, Maseno University, Kondele Kisumu-Busia Rd Maseno, Kisumu, Kenya

**Article History**
**Received:** 22.03.2022
**Accepted:** 25.04.2022
**Published**: 30.04.2022

**Journal homepage:**
https://www.easpublisher.com

**Quick Response Code**

**Abstract:** Wanafunzi wengi nchini Uganda wanachukulia utanzu wa ushairi wa Kiswahili kuwa mgumu na wanapata ugumu katika kujifunza ushairi wa Kiswahili. Ushairi wa Kiganda umekuwa unatendwa vizuri katika mtihani wa kitaifa. Upande wa Kiswahili, kuna ugumu katika ujifunzaji wa ushairi wa Kiswahili na ugumu huu umesababisha matokeo mabaya katika mtihani wa kitaifa katika somo la ushairi wa Kiswahili nchini Uganda. Wanafunzi hawa husomea katika mandhari sawa. Hili linazua swali: kwa nini wanafunzi wanaofanya mtihani wa ushairi wa Kiganda watende vizuri kuliko wanafunzi wa ushairi wa Kiswahili? Makala hii itaweka wazi mambo ambayo ushairi wa Kiswahili waweza kukopa kutoka ushairi wa Kiganda na kujiendeleza. Madhumuni ya makala hii yatakuwa: Kudadavua jinsi ushairi wa Kiganda unaweza kusahilisha mtindo katika ushairi wa Kiswahili kupitia ufunzaji na ujifunzaji na kutathimini jinsi ushairi wa Kiganda unaweza kukuza maudhui katika ushairi wa Kiswahili kupitia ufunzaji na ujifunzaji. Mashairi yalikusanywa kutoka diwani mbili za Kiswahili na mbili za Kiganda. Mashairi 60 yalikusanywa yaani 30 ya Kiganda na 30 ya Kiswahili na 15 yalichaguliwa kutoka kila lugha kwa kutumia uteuzi nasibu. Mashairi yalitolewa kwenye diwani za Kiswahili; "Malenga wa ziwa kuu" na "Malenga wa karne moja" na za Kiganda; "Ab'Oluganda ab'Enda emu" na "Balya n'ensekeezi". Makala hii unafafanua jinsi mwalimu wa ushairi wa Kiswahili anavyoweza kuhamisha maarifa kutoka ushairi wa Kiganda hadi wa Kiswahili. Utamsaidia kuendeleza ushairi wa Kiswahili kuhamisha maarifa ya ujifunzaji na ufunzaji kutokana na ushairi wa Kiganda ili kusahilisha ujifunzaji wa ushairi wa Kiswahili.

**Keywords:** Mtindo, maudhui, ushairi, fasihi, uchanganuzi, mchango.

**Copyright © 2022 The Author(s):** This is an open-access article distributed under the terms of the Creative Commons Attribution **4.0 International License (CC BY-NC 4.0)** which permits unrestricted use, distribution, and reproduction in any medium for non-commercial use provided the original author and source are credited.

## 1.1 Utangulizi

Ushairi ni utungo wa kisanaa unaotumia lugha teule na mpangilio fulani wa maneno badala ya kutumia lugha natharia (mflulizo). Ushairi unaweza kuwa kipera cha fasihi simulizi (nyimbo) na pia katika fasihi andishi kwa sababu mashairi yanaweza kuwasilishwa kwa njia ya kukariri na pia kwa njia ya maandishi. Mashairi yanayoghanwa badala ya kuimbwa huitwa maghani.

Kulingana na Shaban (1958) Ushairi ni sanaa ya vina inayopambanuliwa kama nyimbo, mashairi na tenzi. Zaidi ya kuwa sanaa ya vina, una ufasaha na uteuzi wa wa maneno. Kina ni mlingano wa sauti za herufi. Kwa maneno mengine huitwa mizani ya sauti na ufasaha ni ujumi wa lugha. Mawazo, maoni na fikra za ndani zinapoelezwa kwa muhtasari wa shairi huvutia kwa namna ya ajabu

Ushairi ni hifadhi ya asili inayoeleweka zaidi na moyo wa kila mtu anayeishi katika jamii inayohusika (Mwashinga 1997). Ushairi ni msingi wa maneno ya hekima tangu kale. Ndicho kitu kilicho bora sana katika maongezi ya dunia kwa kutumia maneno ya mkato na lugha nzito yenye kunata iliyopangwa kwa urari wa mizani na vina maalumu kwa shairi (Mnyampala 2000).

Utungo ambao katika kila ubeti wake kuna ulinganifu wa vina vitukufu vilivyopangwa kimoja baada ya chenziye; wenye vipande vilivyo na ulinganifu wa mizani zisizo pungufu wala zilizo zaidi; na vipande hivyo viwe vimetandwa na maneno ya mkato maalum na yenye lugha ruwaza, tamu na laini, lugha ambayo ni telelezi kwa ulimi kwa kuitamka, lugha ambayo ina uzito wa fikra, tamu kwa mdomo wa kuisema, tumbuizi kwa masikio ya kuisikia na yenye kuathiri moyo



***Corresponding Author:** Atukunda Edwine
Postgraduate Student, Maseno University, Kondele Kisumu-Busia Rd Maseno, Kisumu, Kenya

uliokusudiwa na kama ulivyokusudiwa (Abdilatif Abdallah 1973).

**1.2 Historia fupi ya Buganda**

Rais (2013) Anasema kuwa Baganda ni kabila mojawapo la makabila yanayopatikana nchini Uganda, na linajumuisha asilimia 16.7 ya jumla ya watu nchini Uganda. Jamii ya Baganda inayo jumla ya koo 52 na ndiyo jamii yenye ufalme mkubwa na wenye nguvu zaidi ya yote nchini. Ni jamii linaloongozwa na Mfalme Ronald Muwenda Mutebi. Neno Uganda lilitokana na utohozi wa Kiswahili uliofanywa na watawala Waingereza mnamo mwaka wa 1884 walipoanza "himaya ya Buganda" Baganda huzungumza Luganda ambayo ni mojawapo ya lugha za Kibantu zinazotokana na jamii kubwa ya Wabantu iliyotoka Kongo.

Lugha ya Kiganda hutofautishwa na lugha zingine za jamii ya kinaija Kongo kwa matumizi ya mihemko katika matamshi. Lugha ya Kiganda ni tajiri hasa katika matumizi ya methali, jazanda, nahau na kadhalika. Mashairi hasa hutumiwa kuhifadhi utamaduni wa Waganda na kwa kiasi fulani historia yao. Kwa hivyo Makala hii inachunguza jinsi Kiswahili kinavyoweza kunufaika katika utajiri huu hasa kishairi. Yaani unaeleza jinsi ushairi wa Kiganda unavyoweza kuchangia katika kuendeleza ushairi wa Kiswahili kupitia ufundishaji.

Lugha ya Kiganda inazungumzwa katika maeneo ya mkoa wa katikati wa nchi ya Uganda ikipakana kaskazini mwa ziwa Victoria, kusini mwa ziwa Kyoga na mashariki ikiwa ni mto Nile.

**1.3 Mchango wa ushairi wa Kiganda katika kuendeleza ushairi wa Kiswahili kimtindo.**

Ushairi wa Kiganda unaweza kuchangia katika kuendeleza ushairi wa Kiswahili kimtindo. Makala hii inatathimini na kufafanua jambo hili kama ifuatavyo:

**1.3.1. Takiriri**

Ni mbinu ya kurudia rudia neno moja au kifungu cha maneno ili kusisitiza ujumbe fulani. Takiriri ilijitokeza kama ifuatavyo katika mashairi ya Kiganda na Kiswahili;
Katika shairi la "lujuuju", kuna takriri kama:
Katika ubeti wa tatu kuna
*"ne"* pia *"nge"* pia neno *"omwenge"*
Maneno haya yamerudiwa rudiwa. Katika shairia la "*nantagwa malambula"* vilevile kuna takriri;
*"ye wuuyo"*

Katika ubeti wa kwanza imerudiwa mara mbili. Vile vile, katika shairi la "okufa nnaku" Kuna neno *"okufa"* katika ubeti wa saba pia kuna *"kuleeta"* katika ubeti huo huo. Pia kuna *"abalala".* Katika shairi la "leeta peesa", Kirai "*leeta peesa"* kimekaririwa. Vile vile katika shairi la "*naawe weebuuze"*, kuna Neno *"kati'* limekarinwa katika ubeti wa tano kuanzia mshororo wa tano hadi wa mwisho. Pia kuna neno *"buli"* katika mishororo yote. Katika shairi la "*banakibuga obuyonjo"* kuna *"Bannange"* katika mshororo wa kwanza na wa pili *"kakunyumya"* katika ubeti wa pili na kadhalika Maneno ya mwisho wa mshororo. Katika shairi la "*omusomesa taata"; "Nze nkutenda"* imerudiwa mara tatu. *"Ng'eby ……."* Inarudiwa mara nne. Katika shairi la "*taata abawo" "Ne tujurira obeewo*" imerudiwa katika ubeti wa kwanza na wa pili.
*"Ne bankikira ensingo"*
*"Ne basikattira balabe*
*"Ne bagikiika ensingo*
*"Bwe tuuyonse ffenna"*

Katika shairi la *obudde buwungeera"* kuna;
***"****Obudde buwungeera"* imekariiwa katika kiia ubeti mshororo wa kwanza.

Katika shairi la **Buganda ejja mu Yuganda ejja**
Misitari hii imekaririwa katika kila ubeti
*"Abantu ba Buganda muluwa"*
*"Abantu ba Buganda weetuli"*
***Tafsiri;*** *Watu wa Buganda muko wapi*
*Watu wa Buganda tupo*

Mbinu hii inajitokeza katika mashairi tisa kati ya mashairi kumi na tano. Hii ni ishara kwamba mbinu ya takiriri inatumiwa sana katika mashairi ya Kiganda kuliko zile mbili ambazo tumeshaona yaani methali na jazanda.
Upande wa ushairi wa Kiswahili, Takiriri inajitokeza kama ifuatavyo;
Katika shairi la **yatakoma**
*Ati ati*, katika mshororo wa kwanza, ubeti wa nne.
Katika shairi la **lililokuudhi ni lipi**
*Lililo langu ni lako, na lako ni langu piya*, mshororo wa kwanza, ubeti wa kwanza.
Katika shairi la **siwanie ukuu,** kuna;
*Juu juu*, mshororo wa kwanza ubeti wa tatu.

Mbinu hii minajitokeza katika mashairi tatu juu ya kumi na tano yaliyoshughulikiwa katika utafiti huu.

Kwa hivyo, mbinu hii inajitokeza sana katika mashairi ya Kiganda kuliko mashairi ya Kiswahili. Katika mashairi ya Kiganda, inajitokeza katika mashairi tisa na katika mashairi ya Kiswahili inajitokeza katika mashairi matatu. Kwa hivyo hii ni tofauti kubwa baina ya mashairi ya Kiganda na Kiswahili. Mashairi ya Kiganda yanasisitiza sana hoja yaani takiriri ni ishara kuwa yanasisitiza sana kuliko yale ya Kiswahili. Ingawa mashairi ya lugha zote yanatumia takiriri, ushairi wa Kiganda unakariri sana kuliko ushairi wa Kiswahili. Pia walimu wote wa Kiswahili walisema kuwa mbinu hii ni rahisi kwa wanafunzi kuelewa. Walimu wa Kiganda pia walisema hivyo wote. Mbinu hii ni rahisi na hujitokeza sana katika ushairi wa Kiganda inamaanisha kuwa ushairi wa Kiganda unatumia sana mbinu rahisi kuliko ushairi wa

Kiswahili. Pia kukariri hurahisisha ujumbe, kwa hivyo ushairi wa Kiganda ukitumia takiriri sana, ujumbe wake huwa rahisi kueleweka.

Kwa hivyo mwalimu wa ushairi wa Kiswahili anastahili kurudia rudia, yaani kukariria wanafunzi wake ili kuwarahisishia kazi. Takriri huwarahisishia kazi na kumuonyesha mwanafunzi ujumbe unaowekewa msisitizo. Kwa hivyo pia mwalimu wa Kiswahili akisisitiza sehemu zenye ujumbe mhimu kwa kukariri sehemu hizi itakuwa rahisi kwa wanafunzi kuelewa ujumbe ulio katika ushairi.

Mashairi ya Kiganda yanatumia takriri kuliko ya Kiswahili. Kulingana na Theodore (1960) anasema kuwa takriri hufanya ujumbe muhimu wa ushairi kutambulika kiurahisi kwa hadhira, yaani inakuwa rahisi kwa hadhira kutambua kiini cha shairi kwa kuangalia sehemu ambazo malenga amewekea msisitizo kwa kuzikariri. Kwa hivyo, kwa kutumia sana takriri, mashairi ya Kiganda yanakuwa rahisi kueleweka kwa wanafunzi kuliko yale ya Kiswahili.

Peter (1987) anasema kuwa takriri husaidia shairi kuwa na muwala, huletea hoja za mashairi kutambuliwa upesi na kufuatana ifaavyo, ili hadhira izielewe upesi na haraka. Kwa uwepo wa takriri nyingi katika mashairi ya Kiganda, huyarahisisha kwa hadhira, yaani wanafunzi wa ushairi wa Kiganda. Anatoa mfano wa jinsi wimbo anavyofanya mtoto alale au anyamanze aliapo unaporudiwa rudiwa. Takriri huvutia sana hadhira na kuburudisha akili ya msomaji au msikilizaji. Kwa hivyo mashairi yakitumia sana takriri yanaburudisha na kuvutia. Kwa hivyo mashairi ya Kiganda kwa kutumia sana takriri kuliko ya Kiswahili, yanavutia wasomaji kuliko ya Kiswahili na fasihi inahitaji hadhira humakinika. Kwa hivyo ili ushairi wa Kiswahili kushika makini lazima uvutie hadhira yake.

Daniel (1972) anasema kuwa ni rahisi kwa mtu kukumbuka jambo linapokaririwa. Anasema kuwa washairi hukariri ujumbe ili ujumbe wao ukumbukwe na hadhira. Kwa hivyo, ni rahisi kwa wanafunzi wa Kiganda kukumbuka ujumbe kwa sababu ya takriri nyingi zinazotumika katika ushairi wa Kiganda. Kwa upande wa Kiswahili, takriri haitumiki sana na hii ni sababu kwa nini wanafunzi wa ushairi wa Kiswahili hupata ugumu kukumbuka ujumbe wa mashairi katika mitihani.

Anaongeza kuwa takriri hulipa shairi mdundo na kulifanya liimbike kwa urahisi. Uimbikaji wa shairi huvutia sana hadhira na pia hurahisisha ukumbukaji wa ujumbe. Uchunguzi huu umegundua kuwa malenga wa Kiganda huweka msisitizo wao kwenye uimbikaji wa mashairi ndiyo sababu mashairi ya Kiganda yanatumia sana takriri kuliko ya Kiswahili. Haya yote yanasahilisha ushairi wa Kiganda na kwa hivyo unawavutia sana wanafunzi kuliko ushairi wa Kiswahili. Ndiyo sababu wanatenda vizuri sana katika mtihani kuliko ushairi wa Kiganda.

**1.3.2 Nahau**

Nahau ni semi fupi fupi anbazo hutumia lugha au maneno ya kawaida lakini maneno hayo hutoa maana tofauti na ile iliyo kwenye maneno ya awali.
Katika shairi la ***"lujuuju"*** kuna misemo kama;
Ubeti wa kwanza kuna *"laba bwe yeekatankita obugiraasi?"*
*Ona jinsi anavyo kunywa birauli za pombe*

*"Ekonko-etakula"* katika shairi la "nantagwa malambula" vile vile kuna nahau kama *"Nantaggwa malambula"* utamu wake hawishi katika ubeti wa kwanza pia kuna *"Nnyabo mutambuza ddembe"* yaani anayetembea vizuri. Pia kuna *"Ne nneesunako"*. Pia katika shairi la "leeta peesa", kuna nahau kama *"ngeri ki n'omegga ate n'okuluma"* yaani kumdharau sana *"ansaba peesa n'ekifuba"* yaani anaomba pesa kwa nguvu. Pia katika shairi la "*okufa nnaku"* kuna; *"Ebeera mbaga yennyini"* yaani' *'huwa kuna arusi"* kumaanisha kwamba huwa kuna shughuli. Pia kuna *"okufa kuzaala eminyira"* na *"abalala bagenda kipayopayo"* hizi nahau zimetumika kurejaea kifo. Katika "*buyonjo zikalina"* kuna *"Akagatto akasimbye"* yaaani amevaa kiatu. *"Nantanyweza bisibe"* yaani hawezi kujizuia. Katika shairi la *taata abawo* kuna
*"Bwetusikesa emikono"*
*"Ne bankiikira ensingo"*
*"Bwe tuuyonse ffenna"*
*"Okuwona zino enkonge"*

Katika shairi la "*bannakibuga obuyonjo*", kuna *"ajula abula"* katika mshororo wa tatu ubeti wa pili.
*"Bumali abayitaba!"*
***Tafsiri;*** *Pesa huwaitikia*
katika shairi la *ensi n'emala ekyuuka* kuna
"*Okutu ne kukira ekkonde'*
*"Amerika Libiya guzisaza mu kabu*
*"Kwagalana na kussa kimu"*
***Tafsiri;*** *Sikio huwa kubwa kuliko ngumi*
*Malekani na Libiya wakipendana sana*
*Wakipendana na kushirikiana*
katika shairi la *omusomesa taata kuna"ntunwa ng'omuntu" "N'obasomesa ejjengo"*
Katika shairi la **Buganda ejja mu Yuganda ejja** kuna misemo hii;
*"Ka bafuuke abasajja ebyasi"*
*"Tuzimbire Buganda erinya"*
***Tafsiri;*** *Wamekuwa wanaume kamili*
*Tujenge jina la buganda*
Katika shairi la **Mmengo ne kampala obudde bukedde**, kuna;
*"Temwekomya bya bandi"*
*Msichukue vitu vya wengine*
akiwaonya dhidi ya kuchukua vitu vya wengine
*"Abanaalimanga akambugu"*
***Tafsiri;*** *Watakao shirikiana pamoja (lima pamoja)*
yaani wanaoshirikiana na kufanya kazi pamoja.

Pia kuna; *Buganda eradde*
*Buganda iko salama*

Mbinu hii inapatikana katika mashairi kumi na moja ya kiganda miongoni mwa kumi na tano yaliyoshirikishwa katika utafiti huu.
Katika mashairi ya Kiswahili, misemo hii ilipatikana;
Katika Shairi la ***kijungu jiko*** lina semi, kama;
*Hali zetu huzorota* katika mshororo wa kwanza ubeti wa pili
*Nyama za bandi*, mshororo wa pili ubeti wa tatu.
*Isiwajae huzuni* mshororo wa kwanza ubeti wa tano
*Soma kwa makini*, mshororo wa pili ubeti wa tano
*Kufanya tamaa* mshororo wa kwanza ubeti wa nane

Katika shairi la ***mwerevu hajinyowi***
*Kujiona kama ndovu* mshororo wa kwanza kafika ubeti wa kwanza.
*Kisu gutu*, mshororo wa tatu, ubeti wa pili.
*Kujidai mwerevu* mshororo wa mwisho ubeti wa tano.
*Nyama pevu*, mshororo wa tatu, ubeti wa pili

Katika shairi la ***mwanadamu si mtu***
*Kutia a kilini*, mshororo wa pili ubeti wa kwanza

Katika shairi la ***kizazi cha fedheha***
*Kupata dhiki*, mshororo wa tatu ubeti wa pili
*Kubaki nyuma*, mshororo wa pili ubeti wa tatu
*Kulala chali*, mshororo wa tatu ubetiwa tano
*Igeni nyuki*, mshororo wa kwanza ubeti wa nane.

Pia, Shairi la ***jisahihishe*** lina semi kama;
*Nyoyo zao huumia*, mshororo wa tatu, ubeti wa kwanza.
*Nakereketwa mtima*, mshororo wa kwanza ubeti wa nne
*Mwenye damu sio chaana* mshororo wa tatu ubeti wa tano.
*Walo juu hurindiona*, mshororo wa tatu ubeti wa sifa.

Pia, shairi la ***kufu la umalenga*** lina semi kama
*Telezi zenye dosari*, mshororo wa tatu ubeti wa tano
*Fikira za kupunga*, mshororo wa mwisho ubeti wa tisa.
*Kupiga chenga* mshororo wa pili ubeti was aba.

Shairi la ***jipi*** lina semi kama
*Kuona mafeso*, mshororo wa tafu ubeti wa pili.
*Jasho jembamba* mshororo wa kwanza ubeti wa kumi.

Shairi la ***semeni wenye kusema***
*Ndimi zenye makali ka wembe*, mshororo wa kwanza ubeti wa kwanza.
*Kimya kama mapunde*, mshororo wa pili ubeti wa kwanza.
*Natiye mpini jembe*, mshororo wa pili ubeti wa sita.
*Wale waliyo simba*, mshororo wa tatu ubeti wa sita.

Shairi la ***wasiwasi nenda zako***
*Kusononeka moyoni*, mshororo wa mwisho ubeti wa tano

Shairi la ***lipi litakalokuwa***
*Tupate tuwa*, mshororo wa tatu ubeti wa kwanza.

Shairi la ***siwanie ukuu***
*Utavunjika maguu*, mshororo wa tatu ubeti wa kwanza.
*Kutafuta ukuu*, mshororo wa pili ubeti wa kwanza
*Ujaze lako bunguu*, mshororo wa kwanza ubeti wan ne.

Shairi la siwi nao lina semi kama
*Wenye ndweo*, mshororo wa pili ubeti wa kwanza
*Wapiga dafurao*, mshororo wa tatu ubeti wa pili
*Kuleta kilio*, mshororo wa tatu ubeti wa tatu

Hii inaonyesha kuwa mashairi ya Kiswahili yanatumia nahau kuliko mashairi ya Kiganda. Mashairi yote ya Kiswahili yaliyoshughulikiwa katika utafiti huu yanatumia misemo. Hii mbinu inajitokeza sana katika ushairi wa Kiswahili. Mbinu hii ilitajwa na walimu wote walioshiriki katika utafiti huu kama mbinu ngumu kwa wanafunzi kuelewa. Kwa hivyo kujitokeza sana katika mashairi ya Kiswahili huyafanya magumu, kwa kuwa mwanafunzi lazima achambue maana ya misemo ili kupata maana ya shairi zima. Kwa hivyo misemo ikiwa mingi, shairi linakuwa gumu. Mashairi kumi na mawili juu ya kumi na tano yaliyoshughulikiwa yanatumia mbinu hii.

Heathers (2003) anasema kuwa mashairi yanayotumia nahau huwa magumu kueleweka. Yanahitaji kufikiria kwa undani sababu mwandishi amesema alichosema. Anasema kuwa nahau katika mashairi husaidia kuyapa uzito wa lugha unaofurahisha lakini pia unaoficha ujumbe. Inambidi msomaji wa shairi kufikiria sana ili kupata ujumbe unaopitishwa kwake. Mwandishi anaweza akasema jambo kwa kutumia nahau huku jambo hilo likimaanisha kitu kingine kabisa. Kwa hivyo kutumia sana nahau katika mashairi ya Kiswahili huyaletea kuwa magumu kwa hadhira hasa wanafunzi wa ushairi wa Kiswahili. Ujumbe ambao unapitishwa kwa hadhira hufichama katika uzito wa lugha na kuwa mgumu kwa hadhira kuupata. Hii ndiyo sababu wanafunzi wa ushairi wa Kiswahili hupata matokeo mabaya kwa kuwa nahau nyingi zinazotumika zinawapa changamoto na kufanya iwe vigumu kwao kuuelewa ujumbe. Huwa kinyume na ushairi wa Kiganda ambao ni rahisi kuuelewa kwa kuwa nahau hazitumiki sana na ndio sababu wanafunzi wa ushairi wa Kiganda wanatenda zizuri sana.

### 1.3.3 Tashibiha

Hii ni mbinu ya mlinganisho wa vitu viwili vyenye sifa zinazofanana kwa kutumia maneno ya mlinganisho kama; “mithili ya” “mfano wa” na “kama”. Mbinu hii ilijitokeza kama ifuatavyo katika mashairi yaliyoshughulikiwa;
Katika shairi la “lujuuju” kuna tashibiha zifuatazo:
*“N’ayiritira nga bbaasi?”*
***Tafsiri;*** *Anakoroma kama basi*
*“Amatama gakwengererera ng’atalya”*
***Tafsiri;*** *Mashavu yamekuiva kama asiyekula*

pia katika shairi la ***"nantagwa malambula"*** kuna tashibiha kama
*"Walungiwa ng'ekitooke kya ssira"*
***Tafsiri;*** *Ulirembeka kama ndizi ya "ssira"*
*"Lindaaza ng'atamidde"*
***Tafsiri;*** *Ninalala kama mlevi kwa sababu yako*
*"Owunikiriza ng'obutiko obubala"*
***Tafsiri;*** *Unashangaza kama uyoga wenye matunda*
. Kaika shairi la ***"leeta peesa"***, kuna tashibiha kama;
*"Ebyedomola ng'ebisila"*
***Tafsiri;*** *Vinaanguka na kishindo kama shina*
*"Agabwatuka nga laddu"*
***Tafsiri;*** *Yanayolipuka kama radi*
Katika shairi la "bannakibuga obuyonjo" *"Mubyemansiza gy'oba ppamba ffiifi"*. Katika shairi la ***"ensi n'emala ekyuuka"*** kuna;
*"ng'enkuyege z'omu kiswa'*
***Tafsiri;*** *Kama mchwa kwenye kichuguu*.
Katika shairi la ***"omusomesa taata***" kuna; *"ngebyo bukimu "ing'eby'ebitabo….."*
Mashairi sita miongoni mwa kumi na tano yana mbinu hii. Kwa hivyo ni mbinu ambayo inatumika sana katika mashairi ya Kiganda.
Katika mashairi ya Kiswahili, mbinu hii inajitokeza kama ifuatavyo;
Katika ***"yatakoma"***
*Papatawe kama uwa la waridi* mshororo wa pili ubeti wa pili
Katika shairi la ***jipu*** kuna
*"Midamu itiririke kama ng'ombe alonona",* mshororo wa tatu ubeti wa tisa.
Katika shairi la ***Semeni wenye kusema*** kuna;
*"Mu kimya kama mapunde"* mshororo wa pili ubeti wa kwanza

Mbinu hii inajitokeza katika mashairi matatu ya Kiswahili. Hii ina maana kwamba mbinu hii haijitokezi sana katika mashairi ya Kiswahili.

Katika mashairi ya Kiganda, mbinu hii ilipatikana katika mashairi sita kati ya kumi na tano ilihali katika mashairi ya Kiswahili ilipatikana katika mashairi matatatu miongoni mwa yale kumi na tano. Hii ni ishara kwamba mbinu hii inajitokeza zaidi katika mashairi ya Kiganda kuliko yale ya Kiswahili. Walimu wote watano wa Kiswahili walioshiriki kuhojiwa katika utafiti huu, waliiweka mbinu ya tashibiha miongoni mwa zile ambazo ni rahisi kwa wanafunzi kuzielewa. Hii ni ishara kuwa mbinu hii rahisi inajitokeza sana katika ushairi wa Kiganda kuliko wa Kiswahili. Hii ndiyo sababu ushairi wa kiganda ni rahisi kueleweka. Unatumia sana mbinu rahisi. Vile vile walimu wa Kiganda walikubali wote kuwa mbinu hii ni rahisi kwa wanafunzi wa ushairi wa Kiganda kuielewa.

Philip (2019) anasema kuwa anatumia sana tashibiha katika mashairi yake ili kuyarahisisha kwa hadhira. Anasema kuwa tashibiha hurahisisha uelewaji wa ujumbe kwa hadhira. Tashibiha hujenga picha au taswira katika akili ya msomaji mambo mawili yanapolinganishwa. Kwa mfano katika shairi, malenga akisema; "nayirittira nga bbaasi" yaani "anakoroma kama basi" msomaji anapata taswira sikizi ya basi na kuelewa vizuri kuwa mtu huyo alikoroma sana. Kwa hivyo mashairi ya kiganda yanakuwa rahisi kuliko ya Kiswahili kwa kuwa yanatumia sana tashibiha ambazo zinarahisisha sana ujumbe kwa msomaji na kumpa msomaji (wanafunzi) taswira ya kitendo au sifa za mtu au kitu kinachoangaziwa. Pia taswira zinafanya mashairi kuburudisha sana wasomaji wake, jambo ambalo linawavutia na kuwafanya wakumbuke ujumbe vizuri. Kwa hivyo, kadiri malenga anavyotumia tashibiha, ndivyo hadhira inazidi kupata ujumbe vizuri. Wanafunzi wa ushairi wa Kiganda wanaelewa ujumbe wa mashairi yao kiurahisi kuliko wa Kiswahili. Kutokana na sababu hii wanafunzi wa ushairi wa Kiganda wanatenda vizuri katika mtihani wa ushairi kuliko wa Kiswahili.

**1.3.4 Utohozi**

Ni mbinu ambapo maneno hukopwa kutoka lugha nyingine na kuandikwa na kutamkwa kama ya Kiswahili. Yaani kuswahilisha msamiati wa lugha zingine. Mbinu hii ilijitokeza kama ifuatavyo katika mashairi yaliyoshughulikiwa;

Katika shairi la "lujuuju", kuna utohozi kama:
*"Bbomu" 'bbiya" obugiraasi* pia katika shairi la *leeta pee*sa kuna utohozi, kama; *"Leeta peesa"* yaani *"leta pesa"*. Imetoholewa kutoka kwa Kiswahili. Kichwa kizima cha shairi hili kimetoholewa. Pia *"ekitambulizo*" kutoka neno la Kiswahili kitambulisho. Pia kuna neno *"doola"* kutoka neno la kiingereza *"dollar"* pia kuna *"ladio kaseti"* kutoka *"radio casset"* na *"miliyooni"* kutoka *"million"* la kiingerezana *"banka"*. Katika "*buyonjo zikalina"* kuna *"Omutiini"* kutokana na neno la kingereza *"teen"* yaani kijana mwenye umri kati ya kumi na tatu hadi kumi na tisa. Katika "*ensi n,emala ekyuuka"* kuna **"**Bbomu" na "*Ttanka"*
Katika "*abakazi kamuli ka looza"* kuna *"Looza"* badala ya *rose.*
Katika shairi la **Buganda ejja mu Yuganda ejja k**una neno "Yuganda" ambalo limetoholewa kutoka Uganda
Katika shairi la **Mmengo ne kampala obudde bukedde**, kuna;
Neno "Yuda" limetoholewa kutoka jina la kingereza "Judas"
Mbinu hii inajitokeza katika mashairi nane ya Kiganda.
Upande wa Kiswahili, kuna *"ruhu"* katika shairi la ***kizazi cha fedheha.*** Neno hilo limetoholewa kutoka neno la kiarabu.

Kwa hivyo mbinu hii inajitokeza sana katika mashairi ya Kiganda kuliko ya Kiswahili. Hii mbinu ni rahisi sana kwa wanafunzi.

Kwa kuwa ni mbinu rahisi kuelewa, mashairi ya Kiganda yanakuwa rahisi kuelewa. Pia mashairi ya Kiganda yanatohoa hasa kutoka lugha ya Kiingereza ambayo ni mojawapo ya lugha rasmi na hutumika sana

shuleni, kwa hivyo wanafunzi wameitumia tangu shule za chekechea na wanaijua vizuri sana. Katika ushairi wa Kiswahili, asilimia kubwa ya maneno hutoholewa kutoka kwa Kiarabu, lugha ambayo wanafunzi wengi nchini Uganda na hata walimu hawana mazoea nayo. Jambo hili hufanya ushairi wa Kiswahili kuwa mgumu. Kwa hivyo lazima mwalimu wa ushairi wa Kiswahili achukue muda na kuwarahisishia wanafunzi msamiati mpya uliotoholewa kutoka kwa Kiarabu ili wanafunzi wa ushairi wa Kiswahili pia watende vizuri katika mtihani wa ushairi kama wa Kiganda. Urahisi huu wa msamiati ndio unafanya wanafunzi wa Kiganda wajifunzi kiuwepesi ushairi wao.

**1.3.5 Balagha**

Maswali ya balagha au tashititi ni maswali yanayoulizwa na mshairi ingawa jibu linajulikana au hakuna haja ya kuyajibu. Mbinu hii ilijitokeza kama ifuatavyo katika mashairi yaliyoshughulikiwa katika utafiti huu;

Katika shairi la ***"lujuuju",*** kuna maswali ya balagha kama;

*"Laba bweye katankira obugiraasi?"*

*"Omuntu n'ayiritira nga bbaasi?"*

***Tafsiri;*** *Mtu anakoroma kama basi*

Pia katika shairi la "leeta peesa" kuna balagha kama;

*"Omuntu aliwona ddi sematalo w'emmundu n'ensibi?"*

***Tafsiri;*** *Mtu atapona lini hivi vita vya bunduki na pesa* mshororo wa kwanza ubeti wa pili. Pia mshororo wa mwisho katika ubeti wa tano kuna;

*"Gwe ssebo oli wa ngeri ki? Tewazaalibwa mukazi?*

***Tafsiri;*** *Wewe ni wa aina gani? Hukuzaliwa na mwanamke?*

Katika shairi la "*okufa nnakku"* kuna,

*"Kituufu baboola bakaaba?"*

***Tafsiri;*** *Ni ukweli kuwa wanadharau na kulia* na

"*Kituufu basinda banyiiga?"*

***Tafsiri;*** *Ni ukweli wanalalama na kukasirika*

na katika shairi la "*bannakibuga obuyonjo"*, kuna;

*"Okufa kuleeta obunaku?"*

***Tafsiri;*** *Kifo huleta huzuni*

vile vile katika shairi la "*naawe weebuuze"* kuna; Kila mshororo katika shairi hili ni swali la balagha. Kwa mfano mshororo wa kwanza *"Enseera bwesala, buli esala nseera?"* na katika shairi la *"buyonjo zikalina"* kuna *"Akonera zawabu?"*

*"Kalina abituusa?"* Katika "*taata abaawo"* kuna *"Lwe tukoze tutya taata. Okutebenkera mu nsi eno?"*

Katika shairi la *"mukama munene"*, kuna*"wali otudde ne weebuuza, Eyazimba obwengula?*
*Natateekako nkondo?*
*Eyatonda enazaluggya?*
*Empungu ne ggaali?......."*

Shairi zima ni maswali ya balagha.

Katika ushairi wa Kiganda, Mashairi kumi miongoni mwa kumi na tano yana mbinu hii ya maswali ya balagha. Mbinu hii inajitokeza sana katika ushairi wa kiganda kiasi kwamba baadhi ya mashairi hutungwa kwa mbinu hii ya kuuliza maswali kuanzia mwanzoni hadi mwishoni kwa mfano, shairi la *"naawe webuuze"*

*Enseera bw'esala, buli esala nseera?*
*Enkoko bw'ekoka. buli akoka nkoko?*
*Enkolo bw'ekula buli ekula nkolo?*
*Nange bwe ssiba, buli ataba taba?*
*Bw'olaba nkula, buli akula alabwa?*

*Mu nkola ekolwa, buli ekolwa nkola?*
*Mu ssanyu nseko, buli nseko ssanyu?*
*Mu kusala empamyo, buli mpamyo esalwa?*
*Nga tukuba entoli, kati entoli ekubwa?*
*Kati ndabye ennaku, buli nnaku erabwa?*

*Kati njiga ssebo, buli ssebo ayiga?*
*Laba nnyabo ankuba, buli akuba nnyabo?*
*Ensega ng'eseega, buli aseega nsega?*
*Zino eccupa nnene, zonna ennene ccupa?*
*Kati alabye endali, buli ndali erabwa?*

*Ewaffe bafa okufa, buli wali kufa bafa?*
*Endeku zinywa okufa, buli ezinywa ndeku?*
*Kati mmaze okkola, buli akola amala?*
*Leka nnyize eminyira, buli minyira ginyizwa?*
*Ka tutege emmese, buli mmese etegwa?*

*Kati ndaba embaki, buli alabwa mbaki?*
*Laba empale empala, buli muwala mpale?*
*Kati enze nkima, buli agenda akimwa?*

*Zino ennene nkima, buli nkima nnene?*
*Ali ennyuma anyumye, buli ennyuma enyuma?*
*Kati awasa awase, buli awase awasa?*
*Kati azina amanyi, buli amanyi azina?*
*Kati ennene ennemye, ddala ennene erema?*
*Kati nnyabo mmaze, buli amala nnyabo?*
*Kati mmaze mmaze, buli amala amaze?*

*Kati mpala ewaka, buli awaka ewalwa?*
*Kati nkola awabi, buli awabi ekolwa?*
*Omulogo mu ttale, buli ttale erogwa?*
*Otubisi mu ccupa, buli ccupa mbisi?*
*Atamanyi amanye, buli amanyi amanywa?*

Shairi zima kuanzia mwanzoni hadi mwishoni linatumia mbinu hii. Kwa hivyo ni mbinu mhimu katika ushairi wa Kiganda.

Katika mashairi ya Kiswahili, maswali ya balagha hujitokeza kama ifuatavyo;

Katika shairi la *kizazi cha fedheha* ni
*Je hamtaki zetu kauli?*
*Mtu pwe mbali mjimiliki?*

Katika shairi la *semeni wenye kusema* kuna;
*Muko wapi wenye ndimi zenye makaliya wembe?*
*Mwangoja yatimu kumi halafu ndipo mulumbe?*
*Mbona leo hamusemi, mu kimya kama mapunde?* (katika ubeti wa kwanza).
*Ni yupi mwenye kutaka – kama hayo yamkumbe?* (ubeti wa pili)

*Mbona leo ukwetu, twaambizana tusambe?* (ubeti wa tatu)

Katika mashairi ya Kiswahili, mashairi mawili tu kati ya mashairi kumi na tano ndiyo yalikuwa na maswali ya balagha. Kwa hivyo mbinu hii inajitokeza zaidi katika mashairi ya Kiganda kuliko ya Kiswahili. Mbinu hii ni rahisi kueleweka kwa wanafunzi kwa kuwa ni maswali tu. Inajitokeza sana katika ushairi wa kiganda na haijitokezi sana katika ushairi wa Kiswahili. Hii ni sababu mojawapo kwa nini ushairi wa Kiswahili huwa mgumu kwa wanafunzi wilayani mukono kuliko ushairi wa kiganda ambao huwa rahisi kwa wanafunzi. Walimu wote wa Kiganda na Kiswahili walikiri kuwa mbinu hii ni rahisi kwa wanafunzi kuielewa wanapochambua. Inatumika sana katika mashairi ya Kiganda kuliko wa Kiswahili. Hii ni sababu moja kwa nini ushairi wa Kiganda ni rahisi kwa wanafunzi kuliko wa Kiswahili.

Uchunguzi huu umegundua kuwa ushairi wa Kiganda unatumia maswali ya balagha kuliko wa Kiswahili. Beqiri (2018) anasema kuwa swali la balagha ni kauli ya ushawishi ambayo huweza kubadilisha fikira za hadhira bila wao kutambua. Inawashawishi kwa kuwauliza maswali ambayo majibu yake wanayajua na kwa hivyo wanashawishika wenyewe bila malenga kuwaambia kufanya hivyo. Anongeza kuwa maswali ya balagha yanaweza kusaidia mshairi kushirikisha hadhira yake kwa kuwauliza swali ambalo wote tayari wana jibu lake. Kwa hivyo hili linawasisimua na kuwashirikisha kiakili. Huwafanya wafikirie sana na kuuelewa ujumbe uliomo upesi na kwa undani. Huwafanya wafikirie kiundani zaidi mada inayozungumziwa au kuwasilishwa. Huyaweka wazi maudhui ya shairi. Pia huvutia nadhari ya msomaji kwa maudhui mhimu katika shairi. Anasema kuwa pia balagha huwavutia wasomaji kimihemko na kuwavuta ili wahisi kuwa ni sehemu ya kinachosemwa na malenga. Hadhira ikihisi kuwa inashirikishwa, inaelewa vizuri ujumbe kuliko inapohisi kuwa haishirikishwi katika shairi.

Kwa hivyo mashairi ya Kiganda ambayo yanatumia sana maswali ya balagha yanakuwa rahisi kueleweka kwa hadhira ambayo ni wanafunzi wanapofunzwa ushairi. Maswali ya balagha huwafanya watafakari sana na kuwashirikisha kiakili, jambo ambalo linafanya uelewaji wao kuwa rahisi. Mashairi ya Kiganda ni rahisi kuliko ya Kiswahili kwa kuwa yanatumai sana mbinu hii kuliko ya Kiswahili.

### 1.3.6 Uhaishaji

Ni kukipa kitu kisicho na uhai, sifa za kiumbe chenye uhai. Katika utafiti huu mbinu hii ilijitikeza kama ifuatavyo katika mashairi yaliyoshughulikiwa;

Katika shairi la *lujuuju*, kuna mifano kama;

*"Ebinyomo ne bimulingiza mu nyindo"*

***Tafsiri;*** *Wadudu huchungulia kwenye pua yake*

pia katika shairi la naawe webuuze kuna *"Endeku zinywa okufa" "Endeku"* ni kitu ambacho hakina uhai lakini hapa kimepewa uhai na uwezo wa kunywa kama binadamu. Vile vile katika shairi la okufa nnaku kuna *"Okufa kuyigga entondo"* na *"Okufa kuzaala obunaku"* kifo kimehaishwa na kupewa sifa za banadamu kama kuzaa na kukasirika bila sababu. Katika shairi la ***bannakibuga obuyonjo***, kuna *Bumaali abayitaba!* Katika shairi la ***Ensi n'emala ekyuuka*** kuna;

*"Ndiga, ngo bizanyya"*

***Tafsiri;*** *Kondoo na chui wakicheza*

Yaani kondoo na chui wanacheza pamoja. Hiyo ni ishara ya amani. Wanayama hawa wamepewa sifa ya binadamu.

*"Wambwa kkapa ne neekuba akawuna"*

***Tafsiri;*** *Mbwa na paka wanacheza wajificho*

Yaani mbwa na paka wakicheza pamoja, vile vile ni ishara ya uwepo wa Amani duniani. Katika shairi la *obudde buwungeera*

*Ssaawa zee wereekerera*
*Wanjuba mmulaba akkirira*
*Wa wonabikande gy'alya ebiwate*
*Munyeeye zirindirira*

***Tafsiri;*** *Saa zinaenda*
*Bwana jua anateremka*
*Anateremka kichakani*
*Nyota zinangojea*

na kadhalika *"Nebikku bimwenyerera, Nkukunyi zeesungirira"*

Katika shairi la **Mmengo ne Kampala obudde bukedde**, kuna;

*"Ekiseera kituuse, kiyita"*

***Tafsiri;*** *Wakati umefika na kupita*

yaani muda umepewa uhai. Una uwezo wa kutembea na kupita.

*"Ogutima oguzaala"*

***Tafsiri;*** *Roho mbaya inayozaa*

roho imepewa uwezo wa kuzaa

*"Buganda nyaffe"* yaani Buganda ni mama yetu, kumaanisha kuwa Buganda ni chanzo chetu. Yaani Buganda imepewa uwezo wa kuzaa.

Kulingana na mifano hii, mashairi ya Kiganda yanatumia uhaishaji kuliko mashairi ya Kiswahili. Walimu wote walioshiriki katika utafiti huu walikiri kuwa hii ni mbinu rahisi kwa wanafunzi kuelewa. Kwa hivyo, ikiwa inajitokeza sana, katika mashairi ya Kiganda kuliko ya Kiswahili, hii ni sababu mojawapo kwa nini mashairi ya Kiganda ni rahisi na hutendwa vizuri sana katika mtihani wa kitaifa kuliko ushairi wa Kiswahili.

Neil (2020) anasema kuwa uhaishaji husaidia malenga kuweka ubunifu katika shairi lake na kuvutia hadhira. Humpa malenga fursa ya kutoa ujumbe mzito na mwingi kwa kutumia kauli fupi. Huzama sana ndani na upesi katika akili ya msomaji kuliko kauli za kawaida. Kulingana na maoni yake, mbinu hii ikiwa inatumika sana katika ushairi wa Kiganda, inayafanya yaeleweke upesi kuliko ya Kiswahili ambayo hayatumii

sana mbinu hii, hivyo kufanya ushairi wa Kiganda kutendwa vizuri sana kuliko mwenzake wa Kiswahili katika.

Tasfida ni mbinu rahisi kwa wanafunzi kwa hivyo ikiwa inajitokeza sana katika mashairi ya Kiganda kuliko ya Kiswahili, ndiyo sababu mashari ya Kiganda ni rahisi kwa wanafunzi kuliko ya Kiswahili. Kulingana na Judy (2020) tasfida husaidia mwandishi humsaidia mwandishi kusema jambo ambalo lingekuwa mwiko kusema kwa kutumia lugha ya kawaida. Pia anasema kuwa mbinu hii yaweza kuongeza vichekesho kwenye shairi inapotumiwa vizuri. Pia anasema kuwa ina uwezo wa kuvutia wasomaji. Ushairi wa Kiganda unatumia mbinu hii kuliko wa Kiswahili na huvutia wasomaji wake kuliko wa Kiswahili. Ndiyo sababu wanafunzi wa ushairi wa Kiganda wanaupenda na kuutenda vizuri kwa kuwa unatumia mbinu zinazowavutia. Kwa hivyo washairi wa Kiswahili waweza kuongeza utumiaji wa mbinu hii.

**1.4 Lugha kwa jumla**

Lugha inayotumika katika ushairi wa Kiganda kwa jumla ni lugha ya msamiati rahisi. Yaani msamiati ambao ni rahisi kueleweka kwa mwanafunzi. Jambo hili hufanya ushairi wa Kiganda kuwa rahisi kuchambua na kuuelewa kwa mwanafunzi. Lugha ambayo inatumika katika ushairi wa Kiswahili inakaribiana sana na lugha ya nathari. Hili huifanya kuwa lugha rahisi kueleweka kwa wanafunzi. Hii ni sababu mojawapo kwa nini wanafunzi wa ushairi wa Kiganda wanatenda vizuri katika mitihani ya kitaifa ya ushairi.

Upande wa Kiswahili, lugha inayotumika ni ya mkato, tena nzito sana yenye msamiati mgumu. Jambo hili huifanya iwe ngumu kwa wanafunzi ambao wanachambua mashairi ya Kiswahili hasa nchini Uganda wilayani Mukono. Wanafunzi hawa wanaofanya somo hili la ushairi huwa bado ni wapya katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kwa hivyo msamiati huu mpya huwa mgumu kwao kuuchambua na kuuelewa kimaana. Pia msamiati wa ushairi wa Kiswahili hubadilishwa kidogo katika ushairi wa Kiswahili. Msamiati hubadilishwa kitabdila, kiinkisari na kimazida. Hili hufanya lugha hii ya ushairi na msamiati wake iwe mpya kwa wanafunzi ambao bado wanajifunza lugha ya kawaida. Na mwishowe hili huwaathiri katika uchambuzi na uelewaji wa maana ya ushairi wa Kiswahili na kuathiri utendaji wao katika mtihani wa kitaifa kwa njia hasi.

Pia sarufi ambayo inatumika katika ushairi wa Kiswahili ni tofauti kidogo kwa kuwa huzingatia uborongaji wa sarufi. Upande wa Kiganda, sarufi ya kawaida hutumika. Kwa hivyo sarufi ya ushairi wao huwa si tofauti na ile ambayo wanafunzi wamezoea na kwa hivyo kuchambua na kuchanganua ujumbe katika mashairi ya Kiganda huwa ni rahisi kwa wanafunzi wa ushairi wa Kiganda kuliko wale wa ushairi wa Kiswahili.

Pia lugha ya ushairi wa Kiganda ni lugha sanifu tu, yaani watunzi wa mashairi ya Kiganda huzingatia lahaja sanifu ya Kiganda tu. Upande wa Kiswahili, watunzi huchanganya lahaja. Mchanganyiko huu wa lahaja hufanya uelewaji wa mashairi kuwa changamano kwa wanafunzi wa Uganda ambao huwa wamejifunza lahaja sanifu tu. Kwa wanafunzi wa Kiganda utumiaji wa lahaja sanifu tu hurahisisha ushairi wao kwa kuwa huwa wanajifunza lahaja hiyo hiyo sanifu ambayo mashairi hutumia. Wanafunzi wa wilayani Mukono (Kyagwe) wangepata ugumu kuelewa lahaja ya wilayani Masaka (Buddu). Kwa hivyo jambo hili hurahisisha ujifunzaji wa ushairi wa Kiganda. Lahaja sanifu huwarahisishia wanafunzi wa Kiganda uelewaji wa mashairi na upande wa Kiswahili utumiaji wa lahaja zisizo sanifu huchanganya wanafunzi.

Pia mashairi ya Kiswahili huchanganya Kiswahili cha kale na cha sasa. Jambo ambalo halifanywi katika mashairi ya Kiganda. Jambo hili hufanya ushairi wa Kiswahili mgumu kwa wanafunzi nchini Uganda kuuelewa. Na hufanya ushairi wa Kiganda rahisi kwa wanafunzi. Hili hufanya ushairi wa Kiganda utendwe vizuri katika mitihani ya kitaifa. Wanafunzi wa ushairi wa Kiswahili nchini Uganda hawajakuwa kimsamiati kwa hivyo uchanganyaji wa msamiati wa sasa na wa kale huwachanganya wanafunzi na kufanya ujifunzaji uwe mgumu.

Ushairi wa Kiswahili ni tofauti na ushairi wa Kiganda ambao hutumia Kiganda cha kisasa tu. Kwa hivyo ushairi wa Kiswahili waweza kukopa tabia hii. Jambo hili hurahisisha uelewaji wa ujumbe kwa wasomaji. Kwa nini Kiswahili cha kale kitumike kuwaandikia wasomaji wa sasa. Kwa hivyo hili ni funzo zuri kwa malenga wa Kiswahili kutoka kwa malenga wa Kiganda. Ushairi wa Kiswahili ukitumia msamiati wa sasa, utavutia wasomaji wa sasa ambao ndio hadhira lengwa. Hili litaeneza ushairi kwa wasomaji wote badala ya wachache wanaofikiriwa kuwa wenye talanta.

Kwa hivyo ushairi wa Kiswahili, kama ilivyo kwa ushairi wa Kiganda waweza kuachana na lugha ya kale. Kikale kinatumika sana katika mashairi ya Kiswahili swala ambalo linawafanya wanafunzi wapate ugumu katika kuelewa ushairi wa Kiswahili. Katika mashairi ya Kiganda, lugha inayotumika ni ya sasa. Inayoeleweka, kwa wanafunzi ambalo wana chambua mashairi.

Mashairi ya Kiganda yanazingatia sana ujumbe kuliko urembo wa lugha. Katika upande wa Kiswahili, mashairi huzingtia sana urembo wa shairi na lugha yake kiasi kwamba ujumbe huwa mgumu kueleweka. Kwa upande wa Kiganda, msisitizo huwekwa kwa ujumbe na uelewekaji wa ujumbe kwa msomaji. Kwa hivyo kama ilivyo kwa ushairi wa Kiganda. Ushairi wa Kiswahili uweke msisitizo kwenye ujumbe kuliko lugha. Ushairi wa Kiganda waweza

kuchangia kwenye ushairi wa Kiswahili na kuuendeleza kiujumbe. Yaani ushairi wa Kiswahili kama ushairi wa Kiganda uweke msisitizo kwenye ujumbe kuliko urembo na ufinyanzi wa lugha. Ujumbe katika mashairi ya Kiganda huwekewa msisitizo kuliko jambo lingine lolote. Pia huwa unaeleweka moja kwa moja. Kinyume chake ni ujumbe katika ushairi wa Kiswahili ambao huwa umefichama katika urembo wa lugha. Yaani lugha hupewa uzito mwingi sana ambao huubeba ujumbe na kuuficha ama kuufanya mgumu kueleweka. Tahajia za maneno hubadilishwa, sarufi yenyewe hupangwa upya ili kulipa shairi urembo. Jambo hili hutatiza uwelewaji wa ujumbe.

Kwa hivyo kama ilivyo kwa ushairi wa Kiganda, lugha yaweza kupambwa lakini ujumbe ndio sababu ya shairi kuandikwa. Yani lengo mhimu la kuandika shairi ni kupitisha ujumbe kwa hadhira si kurembesha lugha. Kwa hivyo ushairi wa Kiswahili uweke msisitizo kwenye ujumbe kuliko lugha kama ilivyo kwa ushairi wa Kiganda.

Pia ushairi wa Kiganda waweza kupitisha tabia ya kutumia lahaja moja katika utunzi wa mashairi kwa ushairi wa Kiswahili. Kama Kiswahili, Kiganda kina lahaja kadhaa. Kiganda kinachozungumzwa katika eneo la Kyagwe ni tofauti kidogo na kile cha Buddu, Busiro, Kyadondo na kadhalika. Ingawa tofauti hizi za kilahaja zipo. Hawatumii lahaja yao katika utunzi wa mashairi kama ilivyo kwa Kiswahili. Diwani zote ambazo zinajulikana za Kiganda, zinazingatia lahaja rasmi. Hili linasaidia kutochanganya wasomaji ambao huenda hawana uzoefu na lahaja kwa mfano ya kimvita katika Kiswahili. Kwa hivyo watunzi wa Kiswahili kama wale wa Kiganda pia wanafaa kujifunza tabia ya kutumia Kiswahili sanifu tu katika utunzi wao. Mashairi yote yakitumia lahaja moja, yatakuwa rahisi kwa watu wengi kuelewa na hivyo yatapata hadhira kubwa. Hadhira ikiongezeka ushairi utaendelea. Kadri ushairi unavyovutia na kusomwa na watu wengi ndivyo unavyoendelea.

Ushairi wa Kiswahili waweza kukopa kutoka ushairi wa Kiganda matumizi ya lahaja moja iliyo rasmi katika utungaji mashairi. Utafiti huu umegundua kuwa mashairi yote ya Kiganda yanatumia lahaja moja yaani lahaja rasmi ya Kiganda. Katika mashairi ya Kiswahili, baadhi ya lahaja zinazotumiwa si rasmi. Unakuta maneno kama “Mato” “Mtanga” “Mtana” Hili litafanya ushairi wa Kiswahili kuwa rahisi kwa wanafunzi kuelewa. Shule zote hufundisha Kiswahili sanifu, na wanafunzi wote nachini Uganda hujifunza lahaja sanifu lakini inapofika kwenye mashairi, wanafunzi wanakumbana na lahaja zisizo sanifu. Hili linawapa ugumu wa kuelewa mashairi ya Kiswahili. Kwa hivyo ushairi wa Kiswahili waweza kukopa kutoka ushairi wa Kiganda utumiaji wa wa Kiswahili rasmi tu katika utungaji wa mashairi. Jambo hili husaidia kuendeleza ushairi. Ni rahisi ushairi kuendelea ukiwa na mtindo mmoja wa lugha kwa kuwa hurahisisha uelewaji wa ushairi. Watu wengi wanaelewa lahaja sanifu kuliko wanaoelewa lahaja moja kwa hivyo ushairi ukitumia lugha sanifu tu, utakuwa rahisi kwa watu walio wengi kuuelewa.

Lugha ambayo inatumika katika mashairi andishi ya Kiganda inakaribiana sana na lugha ya nathari. Waweza kusema kuwa lugha ambayo inatumiwa katika mashairi ya Kiganda ni lugha iliyo kati ya lugha mkato na lugha ya nathari. Jambo hili linafanya uelewaji wa mashairi kwa wanafunzi rahisi zaide kuliko wale wananojifunza mashairi ya Kiswahili. Wanafunzi wanaelewa lugha ya nathari upesi kuliko lugha ya mkato.

Kuna mfanano wa mbinu za utunzi au tamathali za usemi zinazotumika katika ushairi wa Kiswahili na Kiganda. Lakini vilele kuna tofauti. Asilimia kubwa ya mbinu za utunzi zinajitokeza katika mashairi ya lugha zote mbili. Hii ni ishara kuwa mwalimu wa ushairi wa Kiswahili anaweza kutumia ufanano huo kuwarahisishia wanafunzi wa ushairi wa Kiswahili somo hili. Kwa mfano ili kumfanya mwanafunzi aelewe maana ya methali, aweze kutolewa mfano kutoka lugha yake ya mama-Kiganda. Pia wanafunzi waweza kutolewa mfano wa shairi la Kiganda kwanza na mbinu hizi kuchambuliwa kwanza kutoka shairi la Kiganda ili wajionee jazanda, tashibiha, misemo na kadhalika katika mashairi ya lugha ya mama, kisha badaye wapewe shairi la Kiswahili. Hii huwarahisishia wanafunzi uelewaji wa ushairi wa Kiswahili. Ufanano uliopo waweza kutumiwa na mwalimu kuwaonyesha wanafunzi mambo haya katika lugha yao ya mama. Jambo hili litawarahisishia uelewaji wa ushairi wa Kiswahili.

Kwa kuwa mbinu ya inkisari ni mojawapo ya zinazofanya ushairi wa Kiswahili kuwa mgumu kwa wanafunzi, na kutokuwepo kwake katika ushairi wa Kiganda hufanya ushairi wao kuwa rahisi, Mwalimu wa Kiswahili awaelezee wanafunzi neno asili na jinsi lilivyokatwa na kufupishwa katika inkisari. Mwalimu achukue muda wake na kuwafafanilia maneno haya, kwa kuwaonyesha maneno asili ili wanafunzi wasiaone kama maneno mapya. Vile vile mbinu kama mazda na tabdila zifanyiwe hivi.

Pia uborongaji sarufi umegunduliwa kama mbinu inayofanya ushairi wa Kiswahili kuwa mgumu. Na kutokuwepo kwake kwa Kiganda hufanya mashairi ya Kiganda kuwa rahisi. Kwa hivyo mwalimu wa Kiswahili akiwaonyesha wanafunzi sentensi asili inakuwa rahisi kwao kuelewa maana yake.

Pia mwalimu awasaidie wanafunzi kwa kufafanua maana ya shairi kwa lugha ya nathari. Lugha ya nathari ni rahisi kwa wanafunzi kuliko lugha ya mkato. Utafiti huu umegundua kuwa ushairi wa Kiganda hutumia lugha iliyo karibu sana na ya nathari na jambo hili hufanya ushairi wao kuwa rahisi. Kwa

hivyo mwalimu wa Kiswahili akitumia lugha ya nathari, ushairi wa Kiswahili utakuwa rahisi kwa wanafunzi.

**1.5 Mchango wa maudhui ya ushairi wa Kiganda katika kuendeleza maudhui ya ushairi wa kiganda**

Upande wa maudhui, mashairi ya Kiganda yanazungumzia maudhui/mada ambazo ni rahisi kuelewa kwa wanafunzi wa ushairi nchini Uganda kwa kuwa yanahusisha maisha ambayo wanafunzi wanayajua vizuri. Kwa mfano shairi la *obudde buwungeera* na *banakibuga buyonjo*. Shairi la banakibuga buyonjo, linaelezea hali ya usafi nchini Uganda. Hali ambayo wanafunzi mijini kama Mukono wanaijua vizuri. Kwa hivyo wanapoikuta katika mashairi, huwa ni rahisi kwao kuielewa, kwa hivyo huwarahisisishia uchambuzi wa mashairi. Pia shairi kama *buyonjo zikalina* linaelezea hali ya vyoo ambavyo watu masikini wanaoishi mijini kama Mukono huwa navyo nyumbani kwao. Maudhui kama haya huwa rahisi kwa wanafunzi kuelewa kwa kuwa yanazungumzia hali wanayoiona nyumbani kwao. Pia shairi kama *obudde buwungeera* linaelezea hali ya jioni na jinsi inavyokuwa nchini Uganda. Hali ambayo kila mwanafunzi hujionea kila siku. Upande wa Kiswahili, mashairi yanazungumzia maudhui ambayo yanahusisha mikutadha kutoka nchi za ngambo ambayo wanafunzi nchini Uganda hawajaizoea.

Pia ushairi wa Kiganda unazungumzia mada kama mapenzi ambazo zinawavutia sana wanafunzi. Shairi kama *abakazi kamuli ka looza* na shairi la *nantagwa malambula*, ni mashairi ya kimapenzi. Pia katika diwani zilizoshirikishwa katika uchunguzi huu kulikuwa na mashairi mengine mengi yanayozungumzia mapenzi. Mada ya mapenzi ni mada pendwa katika ushairi wa Kiganda. Mada kama hii ya mapenzi huvutia sana wanafunzi na wasomaji wengine. Pia ni rahisi kwa mwanafunzi kuelewa mashairi ambayo yanazungumzia mada kama hii. Upande wa Kiswahili mashairi yote yaliyoshughulikiwa, kulikuwa na shairi moja ambalo liligusia mapenzi lakini haikuwa dhamira kuu. Pia lilizungumzia mapenzi kwa jumla. Halikuzungumzia mapenzi katika muktadha wa bibi na bwana. Maudhui ya mashairi ya Kiganda yanavutia zaidi kuliko yale ya mashairi ya Kiswahili.

Ushairi wa Kiganda unazungumzia maudhui sahili kwa wanafunzi kwa mfano shairi la *"taata abawo"* na shairi la *omusomesa taata*. Mashairi haya yanazungumzia mapenzi ya baba. Yanamsawiri baba kama mtu ambaye ana uwezo wa kutatua matatizo yote ambayo mtoto wake yuko nayo. Mbele ya mtoto, baba huwa na uwezo huu. Watoto wote hufikiria hivyo. Kwa hivyo mashairi kama haya huwa ni rahisi kwa mtoto kuelewa. Upande wa Kiswahili, maudhui yanayozungumziwa ni ya jumla tu na huenda asilimia kubwa ieleweke zaidi kwa watu wazima kuliko wanafunzi. Usahili huu wa maudhui ya ushairi wa Kiganda, hufanya uchambuzi wa maudhui ya ushairi wa Kiganda rahisi kuliko ya ushairi wa Kiswahili na kusababisha utendaji mzuri katika mitihani ya ushairi wa kiganda kuliko ushairi wa Kiswahili.

Dini ambayo inazungumziwa katika mashairi ya Kiganda ni ya ucha Mungu kwa jumla. Yaani si rahisi kutambau kama ni ya kikristo ama ya kiislamu. Kwa mfano shairi la *mukama munene* linamzungumzia Mungu kwa jumla. Dini zote duniani zinamwamini Mungu ila tu njia na mbinu za kumwaabudu huyo Mungu, na sifa za Mungu huyo na majina yake hubadilika kulingana na dini. Kwa hivyo shairi ambalo linamsifu tu mungu linamvutia kila mwanafunzi na halitamletea fikira hasi. Ilihali upande wa Kiswahili mashairi mengi yanapozungumzia dini huwa ni ya kiislamu. Jambo hili huwapa fikira hasi wanafunzi ambao si waisilamu na kuwafanya wafikirie kuwa hilo shairi ambalo si la dini yao, pia haliwahusu. Watunzi wa mashairi ya Kiganda wanatuzungumzia dini iliyo rahisi kwa kila mtu kuidhania kuwa ni yake. Fikira hasi ambaozo zinatokana na dini katika mashairi zaweza kuathiri uwezo wa mwanafunzi kisaikolojia kuchambua mashairi.

Mandhari katika mashairi ya Kiganda ni sawa na yale ambayo wanafunzi wa ushairi wa Kiganda wamelelewa. Ni mandhari ambayo wanayaelewa sana. Mashairi kama *buyonjo zikalina* na *obudde buwungera*, yanazungumzia mandhari ambayo ni rahisi kwa wanafunzi kuelewa. Ilihali mandhari ya ushairi wa Kiswahili ni mageni kwa wanafunzi wa Kiswahili wilayani mukono. Hii ni sababu mojawapo kwa nini ushjairi wa Kiganda hutendwa vizuri katika mtihani wa kitaifa kuliko ushairi wa Kiswahili nchini Uganda. Ikiwa mambo ambayo yanazungumziwa na malenga ni mambo yanayopatikana katika mandhari ya mwanafunzi, huwa rahisi kwa mwanafunzi kuelewa kuliko yakitoka katika mandhari ambayo hajayazoea.

Uchunguzi huu umegundua kuwa mashairi ya Kiganda huwa rahisi kwa wanafunzi nchini Uganda kwa kuwa wanafunzi wamezoeana na mandhari ambayo yanazungumziwa katika ushairi huu. Kwa hivyo mwalimu ahusishe mandhari ya ushairi wa Kiswahili na mandhari ya nchini Uganda. Awapatie mifano ya sehemu amabazo wanafunzi wanazijua na kuzihusisha na zile ambazo zinazungumziwa katika mashairi.

Pia mashairi kama *"zuukuka yuganda muzzukulu wa Buganda"* ni shairi ambalo lavutia sana wanafunzi ambao ni wa kabila la Baganda. Asilimia kubwa ya wanafunzi wilayani Mukono ni ya Waganda. Kwa hivyo huwa ni rahisi kwao kuvutiwa na maudhui kama haya kuliko maudhui ya Kiswahili ambayo huzungumzia maudhui ya nchi zingine. Kabila la waganda hupenda sana ufalme wao kwa hivyo ujumbe unaozungumzia ufalme wao huwavutia sana. Pia mashairi kama *"Buganda ejja mu yuganda ejja" "mmengo ne kampala obudde bukedde" "Buganda mu yuganda eradde"*. Maudhui yake ni maudhui ambayo huvutia sana kwa wanafunzi wa kabila la Waganda kwa

kuwa Waganda wanajulikana kote kuwa wanapenda ufalme wao

Kijumla, ni rahisi kutambua maudhui au ujumbe mhimu katika mashairi ya Kiganda kuliko mashairi ya Kiswahili. Ujumbe katika mashairi ya Kiganda husemwa moja kwa moja kuliko katika ushairi wa Kiswahili. Maudhui katika mashairi ya Kiswahili hufichwa kidogo lakini ujumbe katika mashairi ya Kiganda hujitokeza na kutambulika moja kwa moja. Ujumbe katika ushairi wa Kiswahili hufichwa sana kwa kuwa watunzi huzingatia sana muundo na mtindo kwa hivyo ujumbe hufichama katika mambo haya mawili. Nadhari ya malenga huvutwa sana na urembeshaji wa shairi kimuundo na kimtindo jambo ambalo hufanya maudhui kufichwa ama wakati mwingine kutojitokeza sana. Kwa mfano ni vigumu kutambua ujumbe mhimu katika shairi la *kufu ya malenga*. Mtunzi aliweka msisitizo wake katika kulirembesha shairi kuliko kutoa ujumbe. Jambo hili hufanya uchambuzi wa maudhui katika mashairi ya Kiganda kuwa rahisi kuliko ushairi wa Kiswahili. Hii ni sababu mojawapo kwa nini ushairi wa Kiganda unatendwa vizuri katika mitihani ya kitaifa kuliko ushairi wa Kiswahili.

Kwa hivyo, baada ya kuona tofauti iliyopo kati ya maudhui ya ushairi wa Kiswahili na Kiganda, iligunduliwa kuwa ushairi wa Kiganda waweza kuchangia katika kwendeleza ushairi wa Kiswahili kimaudhui kama ifuatavyo;

Nchini Uganda, malenga wapya wajitokeze na kutunga mashairi ambayo yanazungumzia maudhui yanayoendana na hali ya maisha nchini Uganda. Tuwe na watunzi ambao wanaelewa hali ya maisha nchini Uganda. Uchunguzi huu umegundua kuwa ushairi wa Kiswahili huwa mgumu kwa wanafunzi wa ushairi nchini Uganda kwa kuwa hali ya maisha inayozungumziwa ni ngeni kwa wanafunzi. Na upande wa Kiganda uchambuzi wa maudhui huwa rahisi kwa kuwa hali ya maisha ni ile ambayo wanafunzi wameizoea. Hii ni kwa sababu ushairi wa Kiganda hutungiwa kwenye mandhari yale yale na watunzi ambao wanayaelewa maisha nchini. Kwa hivyo utokeaji wa malenga nchini Uganda, utasaidia sana katika kuendeleza ushairi wa Kiswahili nchini Uganda. Watunzi wa fasihi nchini Uganda wameupuuza sana uwanja wa ushairi kiasi kwamba miongoni mwa diwani zinazotahiniwa hakuna hata diwani moja ambayo imetungiwa nchini Uganda. Zote zinatoka nje, ilihali upande wa tamthilia na riwaya, kuna vitabu kadhaa ambavyo vinatahiniwa na vimetungiwa nchini Uganda. Kwa hivyo watunzi waendeleze ushairi wa Kiswahili kama ilivyo kwa washairi wa Kiganda ambao wameendeleza ushairi wa Kiganda nchini.

Mada pendwa zishirikishwe sana katika mashairi ya Kiswahili. Mada kama mapenzi zinavutia sana wasomaji. Mambo ya ndoa na familia kwa kuwa kila mtu hutoka kwenye familia, hizo ni mada ambazo zinavutia sana wasomaji. Kwa hivyo watunzi wa mashairi ya Kiswahili wanaweza kujifunza utungaji wa mashairi yenye mada sahili tena pendwa kutoka kwa washiari wa Kiganda. Jambo hili litawavutia wasomaji. Tukivutia wasomaji wengi, ushairi wa Kiswahili utaendelea sana na kuwafikia wasomaji Zaidi nchini Uganda. Ushairi ukivutia wasomaji wengi, inamaanisha kuwa watunzi watatiwa moyo na kwa hivyo ushairi utaendelea sana. Pia mada hizi zitakuwa rahisi kwa wanafunzi kuzisoma na kuzichambua. Hili litaendeleza ushairi wa Kiswahili katika uwanja wa elimu. Jambo lolote likiendelea katika ufundishaji wake, linapitishwa kwa kizazi kipya kupitia elimu. Hayo ni maendeleo.

Pia maudhui ambayo ni sahili kwa wanafunzi yazingatiwe kwa kuwa maudhui sahili yatavutia kizazi kichanga na kusaidia katika kwendeleza mashairi. Kizazi kipya kikichangamkia mashairi, hayo ni maendeleo ya ushairi kwa kuwa hadhira kubwa ndio huendeleza fasihi yoyote ile. Tungo lolote bila hadhira ni upotezaji wa nguvu kwa watunzi. Kwa hivyo ushairi wa Kiswahili ukivutia wasomaji zaidi, utaendelea.

Pia ushairi wa Kiswahili waweza kujifunza kutoka maudhui ya ushairi wa Kiganda kuwa swala la dini huambatana na mihemko ya wasomaji. Kwa hivyo ni lazima dini izingatiwe. Ushairi ukizungumzia dini ya kati bila kuegemea upande wa dini moja, inakuwa rahisi kuvutia wasomaji wa dini zote. Fasihi haina dini ingawa inaweza kuzungumzia dini. Kwa hivyo, ushairi wa Kiswahili utenganishwe na dini ya kiislamu kwa kuwa hadhira yake ni ya dini zote. Kwa hivyo maudhui ya ushairi wa Kiswahili lazima yaendelee na kuhusisha dini zote.

Pia utamaduni unaozungumziwa katika ushairi wa Kiswahili uhusishwe na ule wa mashairi ya Kiswahili. Mifano itolewe kwenye utamaduni wao na kulinganishwa na ile ya utamaduni wa Kiswahili.

**Hitimisho**

Ingawa ushairi wa Kiswahili umeendelea kimuundo, kimtindo na kimaudhui kuliko ushairi wa Kiganda, kuna mambo mengi ambayo ushairi wa Kiswahili waweza kukopa kutoka ushairi wa kiganda na kwa hivyo ukajiendeleza. Utafiti huu umetumia ufundishaji kama njia ya kuonyesha mchango wa ushairi wa kiganda katika kuendeleza ushairi wa Kiswahili kwa kuwa ili jambo lolote lihifadhiwe vizuri na kuendelezwa vizuri, ni lazima lifundishwe kwa kizazi kinachofuata. Pia lazima lifundishwe vizuri. Kwa hivyo utafiti huu uliangalia jinsi muundo, mtindo, na maudhui ya ushairi wa kiganda vilivyo, na vilinganisha na vile vya Kiswahili, kisha ukaonyesha ni yepi ambayo ushairi wa Kiswahili waweza kukopa kutoka ushairi wa kiganda. Hili lilifanyika ili kujibu swali la kwa nini ushairi wa kiganda kiganda unafanywa vizuri katika mitihani ya kitaifa kuliko ushairi wa Kiswahili. Kwa hivyo walimu wa lugha zote mbili walishirikishwa ili kulinganisha ni muundo upi, mtindo upi na maudhui

yepi yaliyo rahisi kufunzwa kwa wanafunzi kati ya ushairi wa Kiswahili na Kiganda.

Walimu wa Kiswahili wakiwafanya wanafunzi wapende ushairi wa Kiswahili kama ilivyo ushairi wa kiganda, ushairi wa Kiswahili utaendelea hasa nchini Uganda hasa wilayani mukono kama ilivyo ushairi wa Kiganda.

Uchunguzi huu umegundua kuwa ushairi wa Kiswahili waweza kuendelezwa sana na ushairi wa kiganda. Pia umeonyesha jinsi mwalimu wa Kiswahili anavyoweza kuhamisha baadhi ya maarifa kutoka ushairi wa Kiswahili na kurahisisha ufunzaji wa ushairi wa Kiswahili. Ushairi wa kiswahili nchini uganda una mengi ya kukopa kwa ushairi wa Kiswahili kama ilivyoonyeshwa kwenye makala hii.

## MAREJELEO


- Abdalla, A. (1973). *Sauti ya Dhiki.* Nairobi: Oxford University Press.
- Abedi, A. (1954). *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Abedi, K. A. (1954). *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*, Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Bukenya, A., & na Nandwa, J. (2000). *African oral literature for schools*, Nairobi longhorn Publishers (k) LTD.
- Bukenya, A., & na Nandwa, J. (2000). *African Ora literature for Schools*; Nairobi: Longhorn Publishers (k) Ltd.
- Bukenya, A. N. W. (1994). *Understanding Oral Literature*; Nairobi: E.A.P Ltd.
- Casey. (2004): *Unlikely Heroes and their roles in Fantasy Literature*, mswada ambao bado Chuo kikuu cha Nairobi ambayo bado haijachapishwa.
- Duff, A., & Maley, A. (2007). *Literature*. Oxford: Oxford University Press.
- Easthope, A. (1983). *Poetry as Discourse.* London: Methuen & Co. Ltd.
- Finnegan, R (1994). *Oral Literature in Africa*. Nairobi, Oxford University Press .
- Finnegan, R. (1970), *Oral Literature in Afrika*, london: Oxford University Press.
- Fraser, G. S. (1970). *Metre, Rhyme and Free Verse.* London: Methuen & Co. Ltd.
- Graham, D. (1968). *Introduaction to Poetry.* London: Oxford University Press.
- Indede, F. (2009). “The Pragmatic of Kiswahili Literary Political Discourse”. *The Journal of Pan African Studies*, 2(8), 107-115.
- Kithaka wa. (1990). *Umbo La Mashairi*. Mwamko 5 [Jarida La Chama Cha Kiswahili Chuo Kikuu Cha Nairobi]: Uk. 80-111.
- Kitula, K., & Amata, K. (2001). *Taaluma ya Ushairi*. Nairobi: Acacia Stantex Publishers.
- Knappert. (1967): *Traditional Swahili Poetry: An Investigation into the Concepts of East Liyongo na Lwanda Magere*. Tasnifu ya Uzamili ya Chuo kikuu cha.
- Mulokozi, M. M., na Kahigi, K. (1976) *Malenga wa bara* E.A.LB, Dares-salaam.
- Massamba, D. P. B., (1983). “Utunzi wa Ushairi wa Kiswahili”. Katika: TUKI (Mhariri). *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili: Fasihi.* III. Dar es salaam: TUKI: 55-94.
- Massamba, D. (1983). *Utunzi wa Ushairi wa Kiswahili*. Fasihi [Makala za Semina ya Waandishi wa Kiswahili III], imehaririwa na Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: Uk. 55-94.
- Mayoka, J. K. (1993). Mgogoro wa Ushairi na Diwani ya Mayoka. Ndanda Mission Press.Tanzania.
- Mayoka, J. M. (1984). *Mgogoro wa Ushairi na Diwani ya Mayoka*. Dar es Salaam: Mberia, Tanzania Publishing House.
- Mohamed, S. A. (1990). *Mbinu na Mazoezi ya Ushairi*. Nairobi: Evans Brothers Ltd.
- Mohamed, S. A. (1995). *Kunga za Nathari ya Kiswahili: Tamthilia, Riwaya, na Hadithi Fupi*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Momanyi, C., & na Maitaria, J. N. (2011). “Dhima ya Kibwagizo Katika Ushairi wa Kiswahili”. *Kioo cha Lugha*, 9(1), 95-103.
- Mulokozi, M. M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili* Dares salaam, Tuki
- Mulokozi, M. M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili.* Dar es salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Mulokozi, M. M., & na Kahigi, K. K. (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*. Dar es salaam: Tanzania Publishing House.
- Wa Mberia. (2003). *Kamusi ya Fasihi-Istilahi na Nadharia*, Nairobi: Focus Publishers.
- Wa Mberia. (2008). *Kanzi ya Fasihi-Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*, Nairobi: Vide
- Wa Mutiso. (1985). *Hurafa na uyakinifu katika utenzi wa Hamziyya*. Tasnifu ya uzamili ya *Waislamu*. mswada ambao haujachapishwa.
- Wallah, Wallah bin. (1988). *Malenga wa Ziwa Kuu*. Nairobi: East African Education Publish
- Wamitila. (2002). *Uhakiki wa Fasihi*: Misingi na vipengele vyake. Nairobi: Phoenix.
- Wamitila. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide.
- Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi-Misingi na Vipengele vyake,* Werner (1932): *Hadithi ya Mikidad na Mayasa*. Amedstead Hemsphire: The Azania Press.
- Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa fasihi Misingi na vipengele vyake*, Nairobi phoenix publishers ltd.
- Wamitila, K. W. (2011). *Luluza lugha, kamuli ya methali*, Nairobi longhorn publishers.
- Wamitila, K. W. (2008). *Kazi ya fasihi misingi ya uchanganuzi wa fasihi*: Nairobi vide-Muwa.


**Cite This Article:** Atukunda Edwine, Deborah Amukowa, Owen McOnyango (2022). Ushairi WA Kiganda Unavyoweza Kuchangia Na Kuendeleza Ushairi WA Kiswahili Kimtindo Na Kimaudhui: Mfano WA Ufundishaji Nchini Uganda. *East African Scholars J Edu Humanit Lit*, 5(4), 116-127.